

Kuhesabu wanyama

-  Zanele Buthelezi, Thembani Dladla, Clare Verbeek
-  Rob Owen
-  Matteo E. Mwita
-  1
-  Kiswahili 



Tembo mmoja anakwenda kunywa
maji.



Twiga wawili wanaenda kunywa maji.



Nyati watatu na ndege wanne nao
wanaenda kunywa maji.



Swala watano na ngiri sita
wanatembea kuelekea kwenye maji.



Punda milia saba wanakimbia
kuelekea kwenye maji.



Vyura wanane na samaki tisa
wanaogelea kwenye maji.



Simba mmoja anaunguruma. Naye
anataka kunywa maji. Nani
anamwogopa simba?



Tembo mmoja anakunywa maji na simba.



Global Storybooks

globalstorybooks.net

Kuhesabu wanyama

✍ Zanele Buthelezi, Thembani Dladla, Clare Verbeek
☒ Rob Owen
☞ Matteo E. Mwita

